
# PAKUA SASA MWENDOKASI APP

Uweze kusafiri na Mabasi Yaendayo Haraka

Download on the App Store | GET IT ON Google Play



## WASILIANA NASI


**WAKALA WA MABASI YAENDAYO HARAKA**

Ubungo Maji, Morogoro Road
**S. L. P** 724, Dar es Salaam
**Simu:** + 255 22 2922 8634/33
**Fax:** + 255 22 92 8635
**Barua pepe:** info@dart.go.tz
au mteja@dart.go.tz

@DARTmwendokasi DARTTV 0800 110 147 www.dart.go.tz

www.dart.go.tz


DART
DAR RAPID TRANSIT AGENCY

DART
DAR RAPID TRANSIT AGENCY




# SAFIRI KISASA

MWONGOZO WA KUTUMIA
**MWENDOKASI APP**

*Usafiri wa Umma Nadhifu*

**Sema kwaheri kwa foleni ndefu za kukata tiketi za karatasi, sema kwaheri kwa usumbufu wa chenji madirishani!**




## Mwendokasi App ni nini?

**Programu tumizi ya Mwendokasi (Mwendokasi App) ni mfumo rasmi wa kielektroniki kwenye huduma za usafiri wa mabasi ya yaendayo haraka jijini Dar es Salaam inayosimamiwa na Wakala wa Mabasi ya Haraka - DART.**

App hii ya Mwendokasi imebuniwa maalum ili kuondoa mifumo ya kizamani ya kukata tiketi za karatasi na hivyo kuwarahisisha abiria namna ya kufikia na kutumia usafiri wa mabasi yaendayo haraka kirahisi zaidi.

Uwepo wa App hii ni sehemu ya mkakati wa serikali wa kuingiza teknolojia ya kidijitali katika sekta ya usafiri wa umma ili kuongeza ufanisi na uwazi hata katika ukusanyaji wa mapato .

Kupitia Mwendokasi App, Abiria anaweza kununua tiketi yake ya safari kidigitali popote alipo bila kulazimika kufika kituoni. Tiketi hii inakuja ikiwa na alama za Msimbokodi unaosomwa na mashine za mageti janja ya kuingilia ndani ya kituo.

Katika App ya Mwendokasi ipo kaunti (waleti) ya Kidijitali inayomuwezesha abiria kuiwekea salio kupitia mitandao ya simu (M-Pesa, Mix by Yas, Airtel Money nk) au benki (Nmb, Nbc nk), na kisha kutumia salio hilo kununua tiketi muda wowote. Aidha, kupitia Mwendokasi App, abiria amewezesha kununua Tiketi za mkupuo (Tiketi 10) kwa wakati mmoja. Jambo linalofaa sana kwa wanafamilia na marafiki wanaosafiri pamoja.

App ya Mwendokasi inamsaidia abiria kuona njia za mabasi (routes), Kituo kilichokaribu , na kupata makadirio ya muda wa safari au kuwasili kwa mabasi ingawa kipengele hiki kinaendelea kuboreshwa.

## Mwendokasi App ina faida zipi?

**Kuokoa Muda:** Hapo awali mfumo wa tiketi wa karatasi ulipokuwa unatumika, abiria walikuwa wakipanga mrefu kwenye foleni ya kukata tiketi hasa nyakati za asubuhi na jioni kwenye vituo vyenye idadi kubwa ya abiria. Lakini sasa mambo yamebadilia kupitia Mwendokasi App kwani abiria hapangi tena foleni ya tiketi.

**Urahisi wa Kupanga Safari:** Kupitia Mwendokasi App, Abiria anaweza kukata tiketi yake akiwa bado yupo nyumbani au ofisini, na akifika kituoni ni anaskani tiketi yake katika geti na kuingia ndani ya kituo tayari kwa safari. Tiketi hii inaisha muda wa matumizi baada ya saa 3 (dakika 180) kupita.

**Usimamizi wa Matumizi:** Mwendokasi App inamsaidia abiria kutunza kumbukumbu ya kiasi gani ametumia kwa usafiri kwa mwezi kupitia historia ya miamala na hivyo kuweza kupanga bajeti yake vizuri.

**Kupanga Bajeti:** App hii inakuwezesha abiria kupanga bajeti ya safari zako iwe kwa wiki, mwezi au mwaka kwani fedha utakayoweka katika Waleti/Akaunti yako ya Mwendokasi App itatumika kwenye kununua tiketi pekee na si kwa ajili ya matumizi mengine.

**Kupunguza Upotevu:** Tiketi ya karatasi inaweza kupotea au kufutika, lakini tiketi ya Mwendokasi App ipo salama kwenye simu yako.

**Inadhibiti upotevu wa mapato kwa Serikali:** Matumizi ya Mwendokasi App yanapunguza upotevu wa mapato ya Serikali (Wakala wa DART) yanayoweza kutokea kwenye usimamizi wa fedha taslimu madirishani.

**Ukusanyaji wa Data:** Mwendokasi App inasaidia Wakala wa DART kujua idadi halisi ya abiria wanaotumia vituo fulani na kwa muda gani, jambo linalosaidia kupanga idadi ya mabasi kulingana na mahitaji.

**Utunzaji wa Mazingira:** Matumizi wa Mwendokasi App inasaidia kwa kiasi kikubwa katika utunzaji wa mazingira katika Vituo tofauti utumiaji wa tiketi za karatasi.

**Kupunguza gharama kwa Wakala :**
Matumizi ya Mwendokasi App yanapunguza gharama za kuchapa tiketi za karatasi na hivyo fedha hizo kutumika katika maboresho mengine ya Usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka.

## MASWALI KUHUSU MWENDOKASI APP

**1. Mwendokasi App inapatikana wapi kwenye Simu Janja yako?**
Utaipata Mwendokasi App kwa kuipakua kwenye simu yako kupitia Appstore kwa mtumiaji wa android na Playstore kwa mtumiaji wa IOS.

**2. Unapataje Mwendokasi App kwenye Simu Janja yako?**

Kwa mtumiaji wa simu ya android fungua google playstore kwenye simu yako na kwa mtumiaji wa simu ya IOS fungua App Store kwenye simu y ako kisha andika Mwendokasi App ili uipakue.

**3. Nawezaje kujisajili kwenye Mwendokasi App?**

(i) Baada ya kuipakua App ya Mwendokasi kwenye simu yako ifungue na uchague lugha uitakayo.

(ii) Kisha bofya sehemu iliyoandikwa “KATA TIKETI” itakutaka uweke namba yako ya simu ili kujisajiri.

(iii)Kisha tengeneza nywira yaani Pasword kisha utatakiwa kurudia tena ili kuthibitisha.

1


2



(iv)Baada yah apo utatumiwa namba za OTP kupitia ujumbe mfupi yaani sms kwenye namba yako ya simu uliyoiweka.

(v) Ingiza namba za OTP, kisha utaingia moja kwa moja kwenye menyu kuu na utaona namba yako ya malipo yaani control number.

1


2



**4. Ni vipi naweza kuweka salio katika App ya Mwendokasi ili niweze kukata tiketi?**

(i) Bofya sehemu iliyoandikwa weka hela.
(ii) Chagua mtandao wako wa simu.
(iii) Weka namba ya kumbukumbu yaani control number
(iv) Weka kiasi cha kulipia
(v) Weka namba ya siri ili kukamilisha malipo.
(vi) Hakikisha umepokea sms mbili, ya kwanza ya kutoka GePG na ya pili ya kutoka kwenye mtandao wako wa simu.

1


2



**5. Salio nililoliongeza kwenye Mwendokasi App nitaliona wapi?**

(xvi)Ingia kwenye Mwendokasi App kisha bofya kwenye kijicho kilichopo upande wa kushoto wa skrini yako ili kuona salio kwenye wallet yako.

**11. Swali: Nini kitatokea nikifuta App kwa bahati mbaya? Pesa zangu zitapotea?**

Hapana. Salio lako halihifadhiwi kwenye simu, bali lipo salama kwenye akaunti yako ya mtandaoni. Ukipakua upya App ya Mwendokasi na kuingiza namba yako ya simu na namba ya siri, utakuta salio lako lipo vilevile kama ulivyoliacha.

**12. Nitawezaje kutangaza biashara yangu kupitia Mwendokasi App?**

Unakaribishwa sana kutangaza biashara yako ili ipate mafanikio kupitia Mwendokasi App ambayo inatumiwa na maelfu ya abiria kila siku. Chakufanya ni kuwasiliana na Idara ya Biashara ya Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka – DART kwa kufika katika Ofisi za Wakala wa DART zilizopo Ubungo Maji, Dar es Salaam kupata maelezo zaidi au kwa baruapepe ya info@dart.go.tz au mteja@dart.go.tz .

**13. Je Ninaweza kununuliwa tiketi kupitia Mwendokasi App?**

Ndiyo mtumiaji wa Mwendokasi App anayo nafasi ya kununua tiketi yake pamoja na kumnunulia mtu mwingine kwa kuchagua sehemu iliyoandikwa mnunulie mwingine kisha aingize namba ya simu ya mtu anayemnunulia pamoja na kituo anachotaka kupandia basi baada ya hapo tiketi itatumwa kwenye simu ya huyo mtu.

**14. Je Rafiki yangu anaweza kuniongezea salio katika Mwendokasi App yangu ili ninunue tiketi?**

Ndiyo Rafiki yako anaweza kukuongezea salio kwa kufungua App yake ya Mwendokasi kisha acahague sehemu ya kuhamisha salio na kufuata hatua ziazofuata.

**16. Je, naweza kuhamisha salio kutoka kwenye Kadi ya Mwendokasi kwenda kwenye App ya Mwendokasi?**

Hapana kwa sasa hii haiwezekani.

**17. Je, naweza kuripoti tukio lililotokea kwenye mfumo wa mabasi yaendayo haraka ambalo sio la kawaida ili Wakala wa DART uchukue hatua?**

Ndiyo, Mwendokasi App kupitia kipengele cha Ripoti Tukio, abiria anapata fursa ya kuripoti tukio au matukio yanayotokea kwenye mfumo wa Mabasi Yaendayo Haraka.







**18. Je,naweza kupata taarifa mbalimbali kutoka Wakala wa DART kuhusu taarifa za dharula zinazotokea kwenye Mfumo wa mabasi yaendayo haraka?**

Ndiyo kupitia kipengele cha usumbufu wa huduma, abiria atapata taarifa mbalimbali kutoka Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka - DART kuhusu taarifa za dharula zinazotokea kwenye Mfumo wa DART.

**19. Je, naweza kupata habari mbalimbali kuhusu Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka?**

Ndiyo kupitia kipengele cha Taarifa, abiria ataona picha na kusoma habari mbalimbali za matukio kuhusu Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka.




**20. Je, nawezaje kuwasiliana na wasimamizi wa Mradi wa mabasi yaendayo haraka?**

Ndiyo, kupitia Kipengele cha Wasiliana Nasi abiria ataweza kuwasiliana moja kwa moja na Wakala wa DART kupitia simu ya bure, barua pepe na fomu maalum.


**21. Je naweza kubadili lugha kutoka Kingereza kwenda Kiswahili?**

Ndiyo, unaweza kubadili lugha, muonekano, kuhariri wasifu, kubadili namba ya siri ya akaunti yako nakadhalika kupitia kipengele cha Mpangilio.




**22. Je naweza kutembelea kurasa za mitandao ya kijamii ya wakala kutokea kwenye Mwendokasi App?**

Ndiyo, kupitia jukwaa la Mwendokasi App, abiria utapata fursa ya kutembelea mitandao ya kijamii ya Facebook, Instagram na Twitter (X) ya Wakala wa DART na kupata habari na elimu mbalimbali kuhusu usafiri wa mabasi yaendayo haraka.




**Hivyo basi ndugu abiria wa Mabasi Yaendayo Haraka wakati wote kumbuka Mwendokasi App si tu chombo cha kukata tiketi, bali ni mabadiliko ya kimfumo yenye lengo la kuifanya Dar es Salaam kuwa mji wa kisasa unaotumia teknolojia kurahisisha maisha ya wakazi na wageni wake.**

# PAKUA SASA MWENDOKASI APP

Uweze kusafiri na Mabasi Yaendayo Haraka

Download on the App Store | GET IT ON Google Play

